Maelezo ya

# Nyakati saba za kanisa

## Sura ya Pili

## Maono ya Patmo

### Yohana Katika Patimo (Ufunuo 1:9-20)

Ufunuo 1:9,

> *"Mimi Yohana, ndugu yenu na mwenye kushiriki pamoja nanyi katika mateso na ufalme na subira ya Yesu Kristo, nalikuwa katika kisiwa kiitwacho Patmo, kwa ajili ya Neno la Mungu, na ushuhuda wa Yesu Kristo."*

Mfuatano huu wa maono ya Ufunuo wa Utu wa Yesu Kristo ulitolewa kwa Yohana wakati alipokuwa amepelekwa kwenye Kisiwa cha Patmo. Kisiwa hiki kidogo kiko maili thelathini kutoka pwani ya Asia Ndogo katika Bahari ya Aegean. Kwa kuwa kilikuwa na miamba na kimejaa nyoka, mijusi na nge, kilikuwa na thamani ndogo ya kibiashara, kwa hiyo kilitumiwa na Dola ya Kirumi kama koloni la adhabu ambapo waliwekwa majambazi sugu, wafungwa wa kisiasa, na kadhalika.

Mtaona ya kwamba Yohana amejielekeza kwa Wakristo kama ndugu katika dhiki. Ilikuwa ni wakati huu ambapo kanisa la mwanzoni lilikuwa likipitia katika mateso makuu. Dini yao haikuwa tu "imenenwa kila mahali" bali watu wenyewe walifungwa gerezani na kuuawa. Yohana, kama wengine wengi, sasa alikuwa akifungwa gerezani kwa ajili ya Neno la Mungu na ushuhuda wa Yesu Kristo. Wakati alipokamatwa, wao walijaribu kumuwua kwa kumchemsha katika mafuta kwa masaa ishirini na manne bila kufanikiwa. Maafisa waliokasirika sana na wasiokuwa na la kufanya basi wakamhukumu kwenda Patmo kama mchawi. Lakini Mungu alikuwa pamoja naye, naye aliachwa kuondoka katika kisiwa hicho na kurudi Efeso ambako aliendelea tena kama mchungaji mpaka wakati wa kifo chake.

Maono ambayo Yohana alipokea yalichukua kipindi cha miaka miwili, BK 95-96. Hayo ndiyo maono yaliyo makubwa sana katika Neno lote. Kitabu kizima kimeandikwa katika mafumbo, na kwa hiyo ndicho lengo la ukosoaji karibu wote pamoja na ubishi. Hata hivyo, kina muhuri wa Mungu juu yake. Hilo linakifanya cha kweli na cha thamani kubwa mno kwa wote wanaokisoma ama kusikiliza kurasa zake takatifu.

### Katika Roho Kwenye Siku Ya Bwana

Ufunuo 1:10,

> *"Nalikuwa katika Roho siku ya Bwana; na nikasikia sauti kuu nyuma yangu, kama sauti ya baragumu."*

*"Nilikuwa katika Roho."* Hilo si la kupendeza? Jamani, ninapenda jambo hilo. Ungeweza tu kuyaita maneno hayo, "Maisha yote ya Kikristo." Kama tutaishi kama Wakristo, hatuna budi kuwa katika Roho WAKE. Yohana hakuwa anazungumza juu ya kuwa katika roho yake mwenyewe. Hilo lisingeleta maono haya. Ilibidi iwe ni Roho wa Mungu. Haina budi kuwa ni Roho wa Mungu pamoja nasi, pia, la sivyo jitihada zetu zote ni za bure. Paulo alisema, "Nitaomba katika Roho, nitaimba katika Roho, nitaishi katika Roho." Kama kuna cho chote kizuri kitakachonijia hakina budi kufunuliwa na Roho, kuthibitishwa na Neno, na kudhihirishwa kwa matokeo yake. Kama vile hakika Yohana alivyohitaji kuwa katika Roho kupokea mafunuo haya makuu kutoka kwa Yesu, tunahitaji kuwa katika Roho kufahamu ufunuo ambao Mungu ametupa sisi kuishi katika Neno Lake, kwa kuwa ni Roho yule yule.

Liangalie namna hii. Watu wengi sana wanasoma Biblia ambapo inasema katika Matendo 2:38,

> *"Tubuni mkabatizwe kila mmoja wenu katika Jina la Yesu Kristo mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu,"*

nao wanapita tu moja kwa moja. Hawalioni. Kama wangeliliona, kwa kuingia katika Roho, wangejua ya kwamba kama wanataka kupokea Roho Mtakatifu, wanapaswa kutubu na kubatizwa katika Jina la Bwana Yesu halafu Mungu angewajibika kulitimiza Neno Lake kwa kuwajaza na Roho Mtakatifu. Wao hawaiingii katika Roho Wake la sivyo jambo hilo lingetukia kwao sawasawa kabisa na Neno lisemavyo. Mwombe Mungu apate ufunuo kwa Roho Wake. Hiyo ndiyo hatua ya kwanza. Ingia katika Roho.

Hebu nitumie mfano mwingine. Tuseme unahitaji uponyaji. Neno linasema nini? Vema, sote tumelisoma mara nyingi, lakini hatukuingia katika Roho tulipolisoma. Je! Tulimwomba Mungu Roho Wake atufundishe ukweli wake halisi? Kama tungelifanya hivyo, tungewaita wazee, tutubu dhambi zetu, tutiwe mafuta na kuombewa, na hilo lingetosha. Huenda lisije mara moja, lakini katika Roho Wake, imekwisha. Hakuna mahakama nyingine ya rufaa. Mungu atatimiza Neno Lake. Loo, tunahitaji kuingia katika Roho, ndipo

mambo yatatendeka. USIANZE NA MATENDO. INGIA KATIKA ROHO HALAFU UINGIE KATIKA HAYO MATENDO NDIPO UONE YALE MUNGU ATAKAYOKUFANYIA.

Je! Umewahi kuona jinsi ulimwengu unavyoingia katika roho ya mambo yaliyo katika ulimwengu? Wao wanaenda kwenye michezo yao ya mpira, mashindano yao ya kimichezo, na adansi zao. Wanaingia katika roho yake. Hawaketi pale kama maua ya ukutani, fimbo za kale zilizokauka. Wanaingia moja kwa moja katika hisia ya mambo na kuwa sehemu ya mambo. Lakini, loo, jinsi wanavyowachukia Wakristo kwa kuingia katika Roho wa Neno la Mungu. Wanatuita washupavu wa dini na watakatifu wanaojifingirisha. Hakuna kitu wasichoweza kufanya kuonyesha chuki yao na kutokubali. Lakini puuza jambo hilo. Unaweza kulitarajia, ukijua linakotoka. Endeleeni tu na muingie katika Roho wa kuabudu.

Roho yetu ni safi. Ni mpya. Ni halisi. Ina kiasi na haina mzaha lakini hata hivyo, imejaa furaha ya Bwana. Mkristo anapaswa kuwa mchangamfu na aliyejaa furaha yake mwenyewe katika Bwana tu kama watu wa dunia walivyo wakati wanaposikia utamu na furaha za dunia. Wakristo na walimwengu wote wawili ni wanadamu; wote wawili misisimko. Tofauti ni mioyo ya Wakristo na mivuto yao huwa tu ni juu ya Bwana wa Utukufu pekee na upendo Wake, ambapo ulimwengu unaridhisha mwili.

Sasa inasema ya kwamba Yohana alikuwa katika Roho katika Siku ya Bwana.

Loo, jamani, hii hapa aya ambayo kwa kweli husababisha mafarakano. Si kwamba ni lazima isababishe, ama inapaswa kusababisha mafarakano, lakini wengine hawaoni tu vile Neno linavyosema hasa.

Kwanza kabisa tunaona watu fulani wazuri ambao wanaita Siku ya Bwana, Siku ya Sabato, ambayo kwao ni Jumamosi. Halafu kuna wengine wanaoiita Siku ya Bwana, Jumapili, siku ya kwanza ya juma. Lakini ingewezekanaje iwe moja ya siku hizi, ama hata hizo mbili zimewekwa pamoja, kwa kuwa Yohana alikuwa katika Roho akipokea maono hayo kwa muda wa miaka miwili. Kwa kweli kilichokuwa kimetukia ni kwamba Yohana alinyakuliwa katika Roho na kupelekwa katika Siku ya Bwana, ambayo ingali inakuja. Biblia inazungumza juu ya Siku ya Bwana ambayo itakuwa katika siku za usoni, na Yohana sasa anaona mambo ya siku hiyo ya usoni. Lakini katika wakati huu, ili tu kutuliza akili zetu, hebu na tuone hasa Sabato ni nini leo.

Sabato, kama tunavyoijua kutoka Agano Jipya, SI kuadhimishwa kwa siku fulani. Hatuna amri hata kidogo ya kushika Jumamosi kuwa Sabato, wala hatuna amri yo yote ya kushika siku ya kwanza ya juma, ambayo ni Jumapili. Hii hapa kweli ya Sabato, ambayo maana yake ni "raha." Ebr. 4:8, "Maana kama Yesu angaliwapa raha (ama siku ya raha), asingaliinena siku nyingine baadaye. Basi imesalia raha (kuishika Sabato) kwa watu wa Mungu. Kwa maana yeye aliyeingia katika raha yake, yeye pia amestarehe katika kazi zake mwenyewe, kama vile Mungu alivyostarehe katika kazi Zake." Je! Mlisikia kifungu hicho muhimu katika sehemu ya mwisho ya kifungu hiki? "Mungu aliacha kazi Zake mwenyewe." Mungu aliwapa Israeli siku ya saba kwa ajili ya Sabato yao, kwa ukumbusho wa kazi Yake ambapo Yeye aliuumba ulimwengu na yote yaliyomo, na kisha akaacha kufanya kazi Zake. Alikoma katika kazi Zake. Yeye alipumzika. Sasa lilikuwa ni jambo zuri kuwapa raha ya Sabato watu ambao wote walikuwa wanakaa mahali pamoja kwa wakati mmoja, ili kwamba wote wapate kuadhimisha siku fulani. Leo hii nusu ya ulimwengu iko katika nuru wakati nusu nyingine iko gizani, kwa hiyo isingefaa kitu hata kidogo. Lakini hiyo ni hoja tu kutoka kwa ya kawaida.

Hebu tuone Biblia inatufundisha nini juu ya raha hii ya Sabato. "Kwa maana yeye aliyeingia katika raha yake." Huku kuingia ndani si kuingia tu ndani, bali kudumu ndani yake, ya ile raha. Ni raha ya milele ambayo kwayo siku ya saba ni mfano tu. Saba' ni kukamilisha. Nane ni siku ya kwanza tena. Ufufuo wa Yesu ulikuwa katika siku ya kwanza ya juma, ikitupa sisi uzima wa milele na raha ya Sabato ya milele. Kwa hiyo tunaona ni kwa nini Mungu asingeweza kutupa siku yo yote ya juma kama Sabato (raha). Sisi 'tumeingia ndani' na 'tunadumu ndani' ya raha yetu, jambo ambalo Israeli hawangeweza kufanya, wakiwa tu na kivuli cha mambo halisi ambayo tunayafurahia. Kwa nini turudi kwenye kivuli wakati tuna jambo halisi sasa?

Jinsi tunavyopokea raha hii, ama Sabato ya daima, ni kwenye mwaliko wa Yesu. Alisema katika Mathayo 11:28,29,

> *"Njoni Kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha. Jitieni nira Yangu, na mjifunze Kwangu;*
>
> *…nanyi mtapata raha (ama kushika Sabato, si siku, lakini uzima wa milele, Sabato) nafsini mwenu."*

Haidhuru umekuwa ukifanya kazi chini ya mzigo wako wa dhambi kwa muda gani, iwe ni miaka kumi, miaka thelathini au miaka hamsini, au zaidi, njoo na maisha yako ya uchovu na utapata raha Yake (Sabato ya kweli). Yesu atakupa raha.

Sasa ni raha gani hasa ambayo Yesu atatoa? Isaya 28:8-12,

*"Kwa kuwa meza zote zimejaa matapiko na uchafu, hata hapana mahali pasafi.*

*Atamfundisha nani maarifa? atamfahamisha nani habari hii? Je! ni wale walioachishwa maziwa, walioondolewa matitini?*

*Kwa maana ni amri juu ya amri, amri juu ya amri; kanuni juu ya kanuni, kanuni juu ya kanuni; huku kidogo na huku kidogo:*

*La, bali kwa midomo ya kusitasita na kwa lugha ngeni atasema na watu hawa;*

*ambao aliwaambia, Hii ndiyo raha yenu (Sabato), mpeni raha yeye aliyechoka (ama kushika Sabato Yake); na huku ndiko kuburudika; lakini hawakutaka kusikia."*

Hapa limetabiriwa papa hapa katika Isaya. Na ilitukia kama miaka 700 baadaye wakati wa Pentekoste wakati wao walipojazwa na Roho Mtakatifu sawasawa kabisa na vile ilivyosemwa ingetukia. Hii ndiyo Sabato ya kweli iliyoahidiwa. Basi walipojazwa na Roho Mtakatifu waliachana na anasa za ulimwengu, matendo yao ya kilimwengu, njia zao chafu. Roho Mtakatifu alitawala maisha yao. Waliingia katika raha. Hiyo hapo raha yako. Hiyo ndiyo Sabato yenu. Si siku fulani, wala mwaka fulani, bali umilele wa kujazwa na kubarikiwa katika Roho Mtakatifu. Ni wewe unayekoma, na Mungu akishughulika. Ni Mungu ndani yako akipenda na kufanya mapenzi Yake mema.

Hebu niseme jambo moja zaidi kuhusu Washikajumamosi wanaodai ya kwamba tunakutana siku isiyo sashihi ya juma wakati tunapokutana Jumapili, siku ya kwanza. Haya ndiyo Justin aliyosema katika karne ya pili. "Jumapili kunafanywa mkutano wa wale wote wanaoishi katika miji na vijiji, na sehemu fulani husomwa kutoka kwenye kumbukumbu za mitume na maandiko yao mradi tu wakati unaruhusu. Wakati kusoma kunapomalizika, askofu huonya na kushauri kwa mahubiri kwamba waige mambo hayo mazuri. Baada ya haya sisi sote tunasimama na kuomba maombi ya pamoja. Katika kufunga maombi, kama vile tulivyokwisha eleza, mkate na divai vinawekwa mbele zetu, na shukrani inatolewa na kusanyiko linaitikia, "Amina." Ndipo vitu hivyo hugawanywa kwa kila mtu nao wanavishiriki na vinachukuliwa na mashemasi na kupelekwa nyumbani kwa asiyekuwapo. Matajiri basi na wanaotaka wanatoa sadaka kwa hiari yao na sadaka hii inapewa askofu ambaye hivyo basi anawapa yatima, wajane, wafungwa, wageni wenye kuhitaji." Kwa hiyo tunaona ya kwamba wale wanaodai ya kwamba kanisa la mwanzoni liliendeleza mapokeo ya Kiyahudi ya kukutana katika siku ya mwisho ya juma hawajui kabisa vile historia inavyosema hasa, na kwa hiyo hawastahili kuaminiwa.

Loo, ili kwamba watu wapate kumjia na kupata raha hiyo. Kuna kilio katika mioyo yote kwa ajili ya raha hiyo, lakini walio wengi hawajui jibu lake. Kwa hiyo wanajaribu kutuliza kilio hicho kwa utaratibu wa kidini wa kuadhimisha siku fulani ama kukubali kanuni za imani na mafundisho ya sharti ya kimadhehebu. Bali wakilikosa jambo hilo, wengi hujaribu kunywa pombe, kulewa, na kila upotovu wa mwili, wakidhani ya kwamba kwa kushiriki anasa za dunia wanaweza kuridhika. Lakini katika hayo hakuna raha. Wao huvuta sigara na kutumia madawa ya kulevya ili kutuliza neva zao. Lakini hakuna raha katika madawa ya duniani. Wanamhitaji Yesu. Wanahitaji dawa ya mbinguni, raha ya Roho.

Ndipo wengi wao huenda kanisani Jumapili. Hilo ni zuri lakini hata huko hawana wazo la jinsi ya kumkaribia Mungu na jinsi ya kumwabudu. Yesu alisema kwamba ibada ya kweli ilikuwa katika Roho na katika kweli, Yohana 4:24. Lakini unaweza kupata ibada ya namna gani katika kanisa linalomjua Mungu kidogo sana hata linamtembeza Baba Krismasi katika Krismasi na keki katika wakati wa Pasaka? Walipata wapi mambo hayo? Waliyapata kutoka kwa wapagani na kuyafanya sehemu ya fundisho la kanisa. Lakini wakati mtu anapomgeukia Bwana na kujazwa na Roho Mtakatifu yeye huacha mambo hayo yote. Yeye ana raha katika nafsi yake. Yeye kweli anaanza kuishi, na kumpenda Mungu na kumwabudu.

Sasa hebu turudi kwenye Maandiko yetu. Tunajua kile Siku ya Bwana isicho. Kama si Jumamosi wala Jumapili, ni kitu gani? Vema, hebu tuliweke hivi. Leo hakika siyo siku ya Bwana. Hii ni siku ya mwanadamu. Ni harakati za mwanadamu, kazi ya mwanadamu, kanisa la mwanadamu, wazo la mwanadamu la ibada, kila kitu ni cha mwanadamu, kwa kuwa ni ulimwengu (cosmos) wa mwanadamu. LAKINI SIKU YA BWANA INAKUA. Naam, ni kweli. Ni kwamba tu wakati huu wa Ufunuo wa Yesu Kristo, Yohana alichukuliwa na Roho na kusafirishwa na Roho kwenye ile Siku Kuu inayokuja. Siku ya Bwana ni wakati ambapo siku za mwanadamu zimekwisha. Falme za ulimwengu huu zitakuwa falme za Mungu wetu. Siku ya Bwana ni wakati hukumu zitakaposhuka, na baada ya hayo unakuja ule utawala wa miaka elfu. Sasa hivi ulimwengu unafanya unalotaka kumfanyia Mkristo. Wanamwita kila namna ya majina mabaya, wakimdhihaki. Bali inakuja ile siku kuu na ya ajabu ambapo watalia na kuomboleza, kwa maana Mwana-Kondoo yuaja katika hasira kuuhukumu ulimwengu. Hapo ndipo wenye haki watakapokuwa na siku yao pamoja na Bwana, kwa maana waovu watateketezwa na wenye haki watatembea juu ya majivu yao kuingia katika ule Utawala wa Miaka Elfu. Malaki 4:3,

*"Nanyi mtawakanyaga waovu, kwa maana watakuwa majivu chini ya nyayo za miguu yenu, katika siku ile nitakapofanya jambo hili, asema BWANA wa majeshi."*

**SAUTI KAMA YA BARAGUMU**

Ufunuo 1:10,

*"...Nikasikia sauti kuu nyuma yangu, kama sauti ya baragumu."*

Yohana alikuwa katika Roho, na alipokuwa katika Roho, aliiona ile siku iliyo kuu na nzuri sana ya Bwana Yesu na uweza Wake wote mtakatifu. Wakati ujao ulikuwa karibu kufunuliwa kwa kuwa Mungu alikuwa anataka sasa kumfundisha. Yohana hakusema ilikuwa ni baragumu. Ilikuwa kama baragumu. Sasa wakati baragumu inapopigwa ina jambo la dharura. Ni kama mpiga mbiu, mjumbe wa mfalme, akija kwa watu. Yeye hupiga baragumu. Ni wito wa haraka. Watu hukusanyika kusikiliza. (Israeli daima ilikusanyika kwa kupigwa kwa baragumu.) Jambo fulani muhimu liko karibu kutukia. "Lisikilize." Kwa hiyo sauti hii ilikuwa na wito ule ule wa dharura kama ilivyokuwa nao ile baragumu. Ilikuwa dhahiri na yenye nguvu, ya kushtusha na ya kuamsha. Loo! laiti tungaliisikia sauti ya Mungu kama baragumu siku hii, kwa kuwa ni 'Baragumu ya Injili' ikitangaza 'Neno la Unabii' kutufanya tuwe macho, na kuwa tayari, kwa ajili ya yale yanayoujia ulimwengu.

**AMRI YA KUANDIKA**

Ufunuo 1:11,

*"Ikisema, Mimi ni Alfa na Omega, wa Kwanza na wa Mwisho: na, Haya uyaonayo, uyaandike katika chuo, ukayapeleke kwa hayo makanisa saba yaliyoko Asia: Efeso, na Smirna, na Pergamo, na Thiatira, na Sardi, na Filadelfia, na Laodikia."*

Hili hapa. Wa Kwanza na wa Mwisho, Alfa na Omega: yaani ni KILA kitu. Mungu mmoja wa kweli. Sauti na Neno la Mungu. Kitu halisi na cha kweli vimekaribia. Ni jambo bora lililoje kuwa katika Roho. Jamani, kuwa katika uwepo wa Mungu na kusikia kutoka Kwake... "Haya uyaonayo, uyaandike katika chuo, ukayapeleke kwa hayo makanisa saba." Ile sauti iliyotangaza Neno Lake katika Bustani ya Edeni na juu ya Mlima Sinai, sauti ambayo ilisikika pia katika utukufu mkuu wa Mlima wa Kugeuzwa Sura, ilikuwa inatangaza mara nyingine tena, na wakati huu kwa yale makanisa saba pamoja na ufunuo mkamilifu na wa mwisho wa Yesu Kristo.

"Andika hayo maono, ewe Yohana. Andika kumbukumbu zake kwa ajili ya nyakati zijazo, kwa sababu ni nabii za kweli ambazo HAZINA BUDI kuja kutimia. Yaandike kisha uyapeleke, yapate kujulikana."

Yohana aliitambua sauti hiyo. Loo! utaitambua hiyo sauti wakati Yeye atakapoita kama wewe ni mmoja wa walio Wake.

**VINARA VYA TAA VYA DHAHABU**

Ufunuo 1:12,

*"Nikageuka niione ile sauti iliyosema nami. Na nilipogeuka, niliona vinara vya taa saba vya dhahabu."*

Yohana hasemi ya kwamba aligeuka amwone yule ambaye alisikia sauti yake, bali aligeuka aione hiyo sauti. Loo, napenda jambo hilo. Akageuka aione hiyo sauti. Sauti na mtu ni kitu kimoja. Yesu ndiye NENO. Yohana 1:1-3,

*"Hapo mwanzo kulikuwako Neno, Naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu.*

*Huyo mwanzo alikuwako kwa Mungu.*

*Vyote vilifanyika kwa Huyo; wala pasipo Yeye hakikufanyika cho chote kilichofanyika."*

Kama kweli unaweza kuliona Neno utakuwa unamwona Yesu.

Wakati Yohana alipogeuka aliona vinara vya taa saba vya dhahabu. Kwa kweli vilikuwa vinara vya taa. Na kulingana na aya ya 20, hayo ndiyo makanisa saba: "vile vinara saba vya taa ulivyoona ni yale makanisa saba." Kuwakilisha makanisa ingekuwa vigumu iwe ni mishumaa. Mshumaa huwaka kwa muda kidogo tu na kisha unakwisha. Unakufa. Haungekuwako tena. Lakini vinara vya taa vina sifa ya kudumu isiyopatikana katika mishumaa.

Kama ungetaka kuona picha nzuri ya hiyo taa, soma habari zake katika Zekaria 4:1-6,

*"Na yule malaika aliyesema nami akanijia mara ya pili, akaniamsha, kama mtu aamshwavyo katika usingizi wake.*

*Akaniuliza, Unaona nini? Nikasema, Nimeona, na tazama, kinara cha taa cha dhahabu tupu, nacho kina bakuli juu yake, na taa zake saba juu yake, tena iko mirija saba ya kuleta*

*mafuta, kwa taa zote zilizo juu yake.*

*Na mizeituni miwili karibu yake, mmoja upande wa kuume wa lile bakuli, na mmoja upande wake wa kushoto.*

*Nami nikajibu, nikamwambia yule malaika aliyesema nami, nikasema, Ee Bwana wangu, vitu hivi ni nini?*

*Ndipo malaika aliyesema nami akajibu, akaniambia, Hujui vitu hivi ni nini?*

*Nikasema, La, Bwana wangu. Akajibu akaniambia, akisema, Hili ndilo Neno la BWANA kwa Zerubabeli, kusema, Si kwa uwezo, wala si kwa nguvu, bali ni kwa 'Roho' Yangu, asema Bwana wa Majeshi."*

*Hii hapa taa nyingine ya dhahabu tupu.* Inawaka sana kwa sababu ina mafuta mengi ambayo inayapata kutoka kwenye mizeituni miwili, ambayo inasimama kila upande. Miti hiyo miwili inawakilisha Agano la Kale na Jipya, na bila shaka mafuta yanaonyesha Roho Mtakatifu, ambaye Yeye pekee ndiye anayeweza kuwapa watu nuru ya Mungu. Yule malaika aliyesema na Zekaria alikuwa ni kama anasema "haya uyaonayo yanamaanisha ya kwamba kanisa haliwezi kufanikiwa kwa jambo lo lote kwa uwezo na nguvu zake lenyewe, bali kwa Roho Mtakatifu."

Sasa chunguza kinara hiki cha taa. Utaona ya kwamba kina bakuli kubwa, ama birika, ambalo liko katikati ya ile mirija saba iliyotoka kwake. Bakuli hili limejazwa mafuta ya zeituni ambayo yanatiririka kupitia kwenye tambi saba ambazo zimewekwa kwenye ile mirija saba. Ni mafuta yale yale yanayowaka na kutoa nuru kwenye ncha ya ile mirija saba. Nuru hii haikuzimika kamwe. Makuhani waliendelea tu kumwaga mafuta kwenye bakuli.

Taa hiyo iliwashwa kwa njia maalum. Kwanza, kuhani alichukua moto kutoka kwenye madhabahu takatifu ambayo hapo awali iliangazwa kwa Moto wa Mungu. Aliwasha, kwanza kabisa, ile taa iliyokuwa imekaa juu ya lile bakuli. Kisha akawasha taa ya pili kutoka kwenye ule mwali wa taa ya kwanza. Taa ya tatu ilipata moto wake kutoka kwenye taa ya pili, kama vivyo hivyo na ya nne ilivyopokea kutoka kwa ya tatu, na kuendelea, mpaka taa zote saba zikawa zinawaka. Moto huu mtakatifu kutoka katika madhabahu, ukipitishwa toka taa hadi taa, ni mfano mzuri sana wa Roho Mtakatifu katika zile Nyakati saba za Kanisa. Kule kumwagwa kwa kwanza kwa Pentekoste (ambapo kumwagwa huko kulitoka moja kwa moja kwa Yesu aliyeketi kwenye Kiti cha Rehema) kunalipa Kanisa Lake nguvu katika nyakati zote saba, na kuonyesha kikamilifu ya kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, na leo, na hata milele, Mungu yule asiyebadilika katika tabia Yake na njia Zake.

Katika Yohana 15, Yesu alisema, "Mimi ndimi Mzabibu, ninyi ni matawi." Yeye ndiye Shina la Mzabibu, ule unaotoka kwenye mzizi wa asili kutoka katika mbegu ya asili iliyo na uhai ndani yake. Sasa mzabibu hauzai matunda; ni matawi ndiyo yanayozaa. Sasa angalia jambo hili: Unaweza kuchukua mti wa jamii ya mbalungi kama vile mchungwa, na kuupandikiza kwenye tawi la mzabibu, tawi la mlimao, tawi la mchenza, na aina nyingine za jamii hiyo, na matawi hayo yote yataota. Lakini matawi hayo yaliyopandikizwa hayatazaa machungwa. Hapana bwana. Limau litazaa malimau, na lile balungi litazaa mabalungi na kadhalika. Hata hivyo matawi hayo yatakuwa yakiishi kwa uhai wa huo mti. Lakini kama mti huo ukipata kutoa tawi lingine lake lenyewe litakuwa tawi la mchungwa na litazaa machungwa. Kwa nini? Kwa sababu uhai uliomo kwenye hilo tawi na uhai uliomo kwenye shina ni sawa lakini sivyo ilivyokuwa kwa matawi yaliyopandikizwa. Hayo matawi yaliyopandikizwa yalikuwa yakitoa uhai wao kutoka uhai wa aina nyingine, kutoka kwenye mizizi mingine, kutoka kwenye mbegu zingine. Loo! yatazaa matunda kweli, lakini hayatazaa machungwa. Hayawezi kwa sababu si ya asili.

Hivyo ndivyo kanisa lilivyo. Mzabibu umepasuliwa na matawi yamepandikizwa. Wamepandikiza matawi ya Kibatisti, matawi ya Kimethodisti, matawi ya Kipresbiteri, na matawi ya Kipentekoste. Na matawi hayo ya nazaa tunda la Kibatisti, Kimethodisti, Kipentekoste, na la Kipresbiteri. (Mbegu za Kimadhehebu ambao kutokana na hizo huzaa matunda yao.) Lakini kama mzabibu huo ukiwahi kutoa tawi lingine lake wenyewe, tawi hilo litafanana kabisa na huo mzabibu wenyewe. Litakuwa tawi kama lile lililozaliwa huko Pentekoste. Litanena kwa lugha, litatabiri, na kuwa na nguvu na ishara za Yesu Kristo aliyefufuka ndani yake. Kwa nini? Kwa sababu linasitawi kwa chakula cha asili cha mzabibu wenyewe. Mnaona, halikupandikizwa kwenye mzabibu; LILIZALIWA katika ule mzabibu. Wakati matawi hayo mengine yalipopandikizwa, yote yaliyoweza kufanya ni kuzaa matunda yao wenyewe kwa maana hayakuzaliwa na mzabibu huo. Hayajui juu ya yale maisha ya asili na tunda la asili. Hayawezi kujua kwa kuwa hayakuzaliwa nao. Lakini kama yangalizaliwa nao, uhai ule ule uliokuwa kwenye shina la asili (Yesu) ungepitia kwao na kudhihirishwa kupitia kwayo. Yohana 14:12,

*"Amin, amin, nawaambieni, Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi, yeye naye atazifanya; naam, na kubwa kuliko hizo atafanya; kwa kuwa mimi naenda kwa Baba Yangu."*

Madhehebu ambayo yanaongozwa na mwanadamu hayawezi kuzaliwa na Mungu; kwa sababu ni

Roho, SI MWANADAMU, anayetoa uzima.

Ni jambo la kusisimua jinsi gani kufikiria juu ya taa hizo saba zikifyonza uhai na nuru kutoka kwenye hazina ya hilo bakuli kuu kwa sababu tambi zao zilikuwa zimetumbukizwa mle. Kila mjumbe wa wakati wa kanisa anaonyeshwa hapa. Maisha yake yamewashwa moto na Roho Mtakatifu. Utambi wake (maisha) umezamishwa katika Kristo. Kwa kupitia utambi huo yeye anafyonza uzima halisi wa Kristo, na kwa huo anatoa nuru kwa ajili ya kanisa. Anatoa nuru ya namna gani? Nuru ile ile iliyokuwa katika ile taa ya kwanza iliyowashwa. Na moja kwa moja katika zile nyakati mpaka wakati huu wa sasa wa mjumbe wa siku ya mwisho maisha yale yale na nuru ile ile inadhihirishwa na maisha yaliyofichwa pamoja na Kristo katika Mungu.

Si kwamba tu tunaweza kunena hivyo juu ya wale wajumbe, bali kila mwamini wa kweli anaonyeshwa waziwazi hapa. Wote wanafyonza kwenye chemchemi ile ile. Wote wametumbukizwa kwenye bakuli lile lile. Wamekufa kwa nafsi zao na maisha yao yamefichwa pamoja na Kristo katika Mungu. Wametiwa muhuri na Roho Mtakatifu. Waefeso 4:30,

*"Wala msimhuzunishe yule Roho Mtakatifu wa Mungu, ambaye kwa Yeye mlitiwa muhuri hata siku ya ukombozi."*

Hakuna mtu awezaye kuwatoa mkononi Mwake. Maisha yao hayawezi kuchezewa. Maisha yanayoonekana yanawaka moto na kuangaza, yakitoa nuru na madhihirisho ya Roho Mtakatifu. Maisha ya ndani, yasiyoonekana, yamefichwa katika Mungu na kulishwa kwa Neno la Bwana. Shetani hawezi kuwagusa. Hata mauti haiwezi kuwagusa, kwa kuwa mauti imepoteza uchungu wake; kaburi limepoteza ushindi wake. Mungu na ashukuriwe, wao wana ushindi huu katika Bwana Yesu Kristo na kwa kupitia Kwake. Amina na amina.

**SI KUHANI TENA**

Ufunuo 1:13,

*"Na katikati ya vile vinara nikaona mtu mfano wa Mwanadamu, amevaa vazi lililofika miguuni, na kufungwa mshipi wa dhahabu matitini."*

Huyo hapo amesimama, Mmoja mfano wa Mwana wa Adamu. Kama vile lulu ilivyo nzuri kwa kutengenezea pete vivyo hivyo Yeye anatukuzwa katikati ya makanisa. , Ni Siku ya Bwana; kwa kuwa Yohana anamwona amesimama, si kama kuhani, bali kama Hakimu anayekuja. Ule mshipi wa dhahabu haufungwi tena kiunoni ambapo kuhani hana budi kuuvaa anapomtumikia Mungu katika Mahali Patakatifu Sana, lakini sasa uko mabegani Mwake, kwa kuwa Yeye sasa si kuhani bali ni HAKIMU. Sasa ndipo Yohana 5:22 imetimia,

*"Tena Baba hamhukumu mtu ye yote, bali amempa Mwana hukumu yote."*

Huduma Yake imekwisha tolewa. Ukuhani umekwisha. Siku za unabii zimekwisha. Yeye anasimama amejifunga kama HAKIMU.

**UTUKUFU WENYE SIFA SABA WA UTU WAKE**

Ufunuo 1 :-16,

*"Kichwa Chake na nywele Zake zilikuwa nyeupe kama sufu nyeupe, kama theluji; na macho Yake kama mwali wa moto.*

*Na miguu Yake kama shaba iliyosuguliwa sana, kana kwamba imesafishwa katika tanuru; na sauti Yake kama sauti ya maji mengi.*

*Naye alikuwa na nyota saba katika mkono Wake wa kuume; na upanga mkali wenye makali kuwili, ukitoka katika kinywa Chake; na uso Wake kama jua liking'aa kwa nguvu zake."*

Jinsi kuonekana kwa Yesu kulivyomvutia na kumtia moyo Yohana, ambaye alikuwa uhamishoni kwa ajili ya Neno, na tazama, NENO Lililo Hai sasa linasimama mbele zake. Ni ono linalotia nuru namna gani, kwa maana kila wasifa wa sifa Zake una maana. Ni ufunuo mzuri ulioje wa Utu Wake mtukufu.

**1 Nywele Zake Nyeupe Kama Sufu**

Yohana kwanza anaona na kutaja weupe wa nywele Zake. Zilikuwa nyeupe, na zenye kung'aa kama theluji. Hii haikuwa ni kwa sababu ya umri Wake. Loo, la. Zile nywele nyeupe na zenye kung'aa sana hazionyeshi uzee bali ujuzi, kukomaa, na hekima. Yule wa Milele haazeeki. Wakati ni nini kwa Mungu? Wakati haumaanishi mengi kwa Mungu, lakini hekima inamaanisha mengi. Ni kama wakati ambapo Sulemani alipomwomba Mungu apewe hekima kuwahukumu watu wa Israeli. Sasa Yeye yuaja, Hakimu wa dunia yote. Atavikwa taji ya hekima. Hiyo ndiyo maana ya nywele nyeupe na zenye kung'aa sana. Tazama hili katika Danieli 7:9-14,

*"Nikatazama hata viti vya enzi vikawekwa, na mmoja aliye Mzee wa siku ameketi, Ambaye mavazi Yake yalikuwa meupe kama theluji, na nywele za kichwa Chake kama sufu safi: kiti Chake cha enzi kilikuwa kama miali ya moto, na gurudumu Zake moto uwakao.*

*Mto kama wa moto ukatoka ukapita mbele Zake: maelfu kumi mara elfu wakamtumikia, na elfu kumi mara elfu kumi wakasimama mbele Zake: Hukumu ikawekwa, na vitabu vikafunuliwa.*

*Nikatazama wakati huo; kwa sababu ya sauti ya yale maneno makubwa iliyoyasema ile pembe; nalitazama hata mnyama yule akauawa, mwili wake ukaharibiwa, akatolewa ateketezwe kwa moto.*

*Na kwa habari za wale wanyama wengine, walinyang'anywa mamlaka yao: walakini maisha yao yalidumishwa kwa wakati na majira.*

*Nikaona katika njozi za usiku, na, tazama, Mmoja aliye mfano wa Mwanadamu akaja pamoja na mawingu ya mbingu, akamkaribia Huyo Mzee wa Siku, wakamleta karibu Naye.*

*Naye akapewa mamlaka, na utukufu, na ufalme, ili watu wa kabila zote, na taifa zote, na lugha zote, wamtumikie: mamlaka Yake ni mamlaka ya milele, ambayo haitapita kamwe, na ufalme Wake ni ufalme usioweza kuangamizwa."*

Hilo hapo. Danieli alimwona akiwa na nywele hizo nyeupe. Yeye alikuwa ni Hakimu akivifungua vitabu na kuhukumu kwavyo. Danieli alimwona akija katika mawingu. Hivyo ndivyo Yohana alivyoona hasa. Wote wawili walimwona Yeye sawa kabisa. Walimwona Hakimu akiwa na mshipi Wake wa hukumu juu ya mabega Yake, akisimama msafi na mtakatifu, amejaa hekima, amestahili kabisa kuuhukumu ulimwengu katika haki. Haleluya.

Hata ulimwengu unafahamu mfano huu, kwa maana katika nyakati za kale hakimu angetokea na kuanzisha mahakama, amevaa wigi nyeupe na nguo ndefu iliyomaanisha mamlaka kamili (vazi refu lililotoka kichwani hadi miguuni) kutoa haki.

**2 Macho Yake Kama Moto.**

Wazia jambo hilo. Hayo macho ambayo wakati mmoja yalififia kwa machozi ya huzuni na huruma. Hayo macho yaliyolia kwa huruma kwenye kaburi la Lazaro. Macho hayo ambayo hayakuona uovu wa wale wauaji waliomsulibisha Yeye msalabani lakini akalia kwa huzuni, "Baba wasamehe." Sasa macho hayo ni mwali wa moto, macho ya Hakimu Ambaye atawapatiliza wale ambao walimkataa.

Katika hisia zote za kibinadamu alizodhihirisha sana kuliko zote wakati alipotokea kama Mwana wa Adamu lilikuwa hili, Yeye alilia mara nyingi. Hata hivyo nyuma ya kulia huko na huzuni hiyo kulikuwa kungali kuna Mungu.

Macho hayo hayo yaliona maono. Yaliangalia ndani katika mioyo ya wanadamu na kujua mawazo yao na njia zao zote mbalimbali. Mungu alikuwa akiangalia kwa macho yawakayo ya kibinadamu, Ambaye aliwaambia wale wasiojua vile alivyokuwa Yeye, "...Msiposadiki ya kuwa Mimi Ndiye, mtakufa katika dhambi zenu." Yohana 8:24.

*"Kama sizitendi kazi za Baba Yangu, msiniamini; lakini nikizitenda, (kazi za Baba Yangu), ijapokuwa hamniamini Mimi, ziaminini zile kazi..."*

Yohana 10:37,38. Kama Yeremia wa zamani, Yeye alikuwa nabii aliaye, kwa maana watu hawakulipokea Neno la Mungu nao waliuwekea kando ufunuo.

Hayo macho yanayowaka moto ya Hakimu yanayowaka kama moto hata sasa yanarekodi maisha ya wanadamu wote. Yakienda mbio huko na huko duniani kote, hakuna kitu asichojua. Yeye anajua shauku za moyo na yale kila mmoja anayotaka kufanya. Hakuna jambo lililofichwa ambalo halitafunuliwa, kwa maana vitu vyote viko tupu machoni Pake Yeye aliye na mambo yetu. Wazia jambo hilo, Yeye anajua hata sasa yale unayowazia.

Naam, Huyo hapo anasimama kama Hakimu mwenye macho makali kama miali ya moto kutoa hukumu. Siku ya rehema imekwisha. Loo! laiti watu wangalitubu na kuutafuta uso Wake katika haki wakati kungali bado kuna wakati. Laiti wangalikifanya kifua Chake mto wa kulalia kabla ulimwengu haujateketea katika moto.

**3 Miguu Ya Shaba.**

"Na miguu Yake ilikuwa kama shaba iliyosuguliwa, kana kwamba imesafishwa katika tanuru." Shaba inajulikana kwa ugumu wake wa ajabu. Hakuna kitu kinachojulikana ambacho kuchanganya nayo ili kuichezea. Lakini shaba hii inayoeleza miguu Yake ingali ni ya ajabu zaidi kwa kuwa imestahimili moto wa

tanuru, jaribio ambalo hakuna kitu kingine kimelipitia. Na hiyo ni kweli kabisa. Kwa maana shaba inaashiria Hukumu ya Kiungu: hukumu ambayo Mungu aliiamuru na kuitimiza. Yohana 3:14-19,

> *"Na kama vile Musa alivyomwinua yule nyoka jangwani, vivyo hivyo Mwana wa Adamu hana budi kuinuliwa:*
>
> *Ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.*
>
> *Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.*
>
> *Maana Mungu hakumtuma Mwana ulimwenguni ili auhukumu ulimwengu; bali ulimwengu uokolewe katika Yeye.*
>
> *Amwaminiye Yeye hahukumiwi: lakini yeye asiyeamini amekwisha kuhukumiwa, kwa sababu hakuliamini Jina la Mwana pekee wa Mungu.*
>
> *Na hii ndiyo hukumu, ya kuwa nuru imekuja ulimwenguni, na watu wakapenda giza kuliko nuru, kwa maana matendo yao yalikuwa maovu."*

Hesabu 21:8, 9,

> *"Bwana akamwambia Musa, Jifanyie nyoka ya shaba, ukaiweke juu ya mti: na itakuwa, kila mtu aliyeumwa, aitazamapo, ataishi.*
>
> *Musa akafanya nyoka ya shaba, akaiweka juu ya mti, hata ikawa, nyoka amemwuma mtu, alipoitazama ile nyoka ya shaba, akaishi."*

Israeli walikuwa wametenda dhambi. Dhambi ilipaswa kuhukumiwa. Kwa hiyo Mungu akamwamuru Musa kuweka nyoka ya shaba juu ya mti, naye aliyeiangalia aliokolewa kutoka katika adhabu ya dhambi yake.

Ile nyoka ya shaba mtini ilikuwa mfano wa dhambi kutoka Bustani ya Edeni, ambako yule nyoka alimdanganya Hawa, akamfanya kutenda dhambi. Shaba inanena juu ya hukumu, kama inavyoonekana katika ile madhabahu ya shaba ambapo hukumu ya dhambi ilitimizwa katika dhabihu juu ya madhabahu. Wakati Mungu alipowahukumu Israeli kwa ajili ya dhambi zao katika siku za Eliya, Yeye aliizuia mvua na mbingu za moto zikawa kama shaba. Sasa katika mfano huu tunaona ya kwamba yule nyoka mtini anawakilisha dhambi iliyohukumiwa tayari, kwa maana imefanywa kwa shaba, ikionyesha hukumu ya Kiungu ilikuwa tayari imeiangukia dhambi. Ndipo ye yote aliyemtazama yule nyoka mtini, akikubali maana yake, alifanywa mzima, kwa maana hii ilikuwa ni kazi ama wokovu wa Bwana.

Nyoka kwenye mti ni mfano wa yale Yesu alikuja duniani kutimiza. Yeye alifanyika mwili kusudi achukue juu Yake hukumu ya Mungu kwa ajili ya dhambi. Msingi wa madhabahu ya dhabihu ulikuwa shaba imara, ikiwakilisha Mwana-Kondoo aliyechinjwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu. Hukumu tayari ilikuwa imepita juu Yake wakati bado hapakuwa na wenye dhambi. Wokovu ukiwa ni wa Bwana kabisa, Yeye alikanyaga shinikizo la ghadhabu ya hasira ya Mungu peke yake. Mavazi Yake yalitiwa rangi nyekundu kwa damu Yake mwenyewe. Tanuru la moto uwakao la hukumu ya haki na ghadhabu ya Mungu vilikuwa fungu Lake. Aliteseka, mwenye haki kwa ajili ya wasio haki.

> *"Umestahili, Ee Mwana-Kondoo wa Mungu, kwa maana umetukomboa kwa damu Yako Mwenyewe."*

"Alijeruhiwa kwa makosa yetu, alichubuliwa kwa uovu wetu, adhabu ya amani yetu ilikuwa juu Yake, na kwa kupigwa Kwake sisi tumepona." Bwana ameweka juu Yake maovu yetu sisi sote. Aliteseka kuliko ambavyo mtu ye yote amewahi kuteseka. Hata kabla ya msalaba Yeye alikuwa ametoa matone makubwa ya jasho kama damu kutoka mwilini Mwake kama vile katika kipeo cha maumivu ya mateso yajayo damu yenyewe ikatengana katika mishipa Yake. Luka 22:44,

> *"Naye kwa vile alivyokuwa katika dhiki akazidi sana kuomba na hari Yake ikawa kama matone ya damu yakidondoka nchini."*

Lakini siku moja miguu hiyo ya shaba itasimama juu ya nchi. Naye atakuwa Hakimu wa dunia yote, Naye atawahukumu wanadamu kwa haki na ukamilifu. Wala hakutakuwako na kuepa hukumu hiyo. Hakuna kugeuza haki hiyo. Hakutakuwa na kuichezea. Mwenye kudhulumu atazidi kudhulumu; mwenye uchafu atazidi kuwa mchafu. Yeye asiyebadilika hatabadilika wakati huo, kwa maana Yeye kamwe hajabadilika wala hatabadilika. Hiyo miguu ya shaba itamponda adui. Itamwangamiza mpinga-Kristo, yule mnyama na ile sanamu na yote yale yaliyo maovu usoni Pake. Ataziangamiza taratibu za makanisa ambayo yamechukua Jina Lake ili tu kupotosha uzuri wake na kuwasagasaga pamoja na mpinga-Kristo. Waovu wote, makafiri, wasiosadiki kuna Mungu, watu wa kisasa, wana mapinduzi, wote watakuwa pale. Mauti, kuzimu, na kaburi vitakuwa pale. Naam vitakuwa pale. Kwa kuwa atakapokuja, vitabu vitafunguliwa. Hapo

ndipo hata kanisa lenye uvuguvugu na wale wanawali watano wapumbavu watakapotokea. Atawabagua kondoo na mbuzi. Wakati atakapokuja Yeye atautwaa ufalme, kwa maana ni Wake, na pamoja Naye watakuwepo maelfu mara melfu kumi, Bibi-arusi Wake, anakayekuja kumtumikia. Utukufu! Loo, ni sasa hivi ama sivyo kamwe. Tubu kabla hujachelewa sana. Amka kutoka katika wafu na ukamtafute Mungu ujazwe na Roho Wake la sivyo utakosa uzima wa milele. Fanya hivyo sasa wakati kungali kuna wakati.

**4 Sauti Yake Ilikuwa kama Sauti ya Maji mengi.**

Sasa maji yanawakilisha nini? Lisikieni katika Ufunuo 17:15,

*"...yale maji uliyoyaona,...ni jamaa, na makutano, na mataifa, na lugha."*

Sauti yake ilikuwa kama sauti ya makutano yakinena. Ni kitu gani? Ni hukumu. Kwa maana hizi ni sauti za makutano ya mashahidi, ambao kwa Roho Mtakatifu katika nyakati zote wamemshuhudia Kristo na kuihubiri Injili Yake. Itakuwa ni sauti ya kila mtu ikisimama katika hukumu dhidi ya mwenye dhambi ambaye hangekubali kuonywa. Sauti za wale wajumbe saba zitasikika kwa sauti kuu na dhahiri. Hao wahubiri waaminifu waliohubiri nguvu za wokovu wa Yesu, waliohubiri ubatizo wa maji katika Jina la Yesu, waliohubiri kujazwa na nguvu za Roho Mtakatifu, waliosimama na Neno kuliko walivyosimama na maisha yao wenyewe; wote walikuwa ni sauti ya Yesu Kristo kwa Roho Mtakatifu katika zile nyakati zote. Yohana 17:20,

*"Wala si hao tu ninaowaombea, lakini na wale watakaoniamini kwa sababu ya Neno lao."*

Umewahi kuwazia jinsi lilivyo jambo la kutisha sana kwa mtu anayechukuliwa na mkondo wa maji bila msaada kuelekea kwenye maporomoko ya maji? Wazia sasa juu ya mngurumo huo anapokaribia maangamizi yake ya hakika na ya kweli. Vivyo hivyo ndivyo hasa ndivyo siku ya hukumu inavyokuja wakati mngurumo wa makutano ya sauti yatakapokuhukumu kwa kutojali kabla haijachelewa. Itilie maanani saa ii hii. Kwa maana wakati huu mawazo yako yanaandikwa mbinguni. Hapo mawazo yako yananena kwa sauti kuu kuliko maneno yako. Kama yule Mfarisayo aliyedai mengi sana kwa mdomo wake, lakini hamsikilizi Bwana, moyo wake ukapotoka na ukawa mchafu hata ikawa amechelewa sana, hata sasa huenda huu ukawa ndio wito wako wa mwisho kulisikia Neno na kulipokea upate uzima wa milele. Utakuwa umechelewa sana utakapokaribia mngurumo wa zile sauti nyingi za hukumu na maangamizi.

Lakini umewahi kuona jinsi sauti ya maji inavyoweza kuwa tamu na ya kuburudisha? Ninapenda kuvua samaki, na napenda kupata mahali ambapo maji yananong'ona katika viwimbi Ninaweza kulala chali tu na kuyasikia yakinena amani na furaha na uradhaa moyoni mwangu. Jinsi nilivyo na furaha kutia nanga katika kimbilio la pumziko ambapo sauti ya Bwana inanena amani, kama vile Neno la maji ya utengano lilivyotangaza. Jinsi tunavyopaswa kushukuru kuisikia sauti Yake ya upendo na uchungaji na uongozi na ulinzi. Na siku moja tutaisikia hiyo sauti tamu ikinena, si katika hukumu, bali katika kutukaribisha sisi ambao dhambi zetu zimeondolewa kwa damu Yake, ambao maisha yetu yamejazwa na Roho, na ambao mwenendo wetu ulikuwa katika Neno. Ni kitu gani kingalikuwa cha thamani zaidi kuliko kusikia sauti nyingi za kukaribisha na kuzungukwa na makutano hao ambao wameamini hadi uzima wa milele? Loo, hakuna kitu kama hicho. Ninaomba ya kwamba utaisikia sauti Yake na usiufanye mgumu moyo wako, bali umpokee kama Mfalme wako.

Loo! laiti tu ungaliliona jambo hilo. Maji ndiyo yaliyouangamiza ulimwengu, lakini yalikuwa ni maji yale yale ambayo yaliyomwokoa Nuhu na pia yakaiokoa dunia yote kwa ajili ya Nuhu. Isikilizeni sauti Yake, sauti ya watumishi Wake, inapowaita kwenye toba na uzima.

**5 Katika Mkono Wake wa Kuume Kulikuwako Nyota Saba.**

"Naye alikuwa na nyota saba katika mkono Wake wa kuume." Sasa bila shaka tayari tunajua kutoka kwenye kifungu cha ishirini nyota hizo saba ni nini hasa. "Na siri ya zile nyota saba ni malaika (wajumbe) wa yale makanisa saba." Sasa tusingeweza kufanya kosa hapa kwa sababu yoyote, kwa kuwa Yeye hutufasiria jambo hilo. Hizi nyota saba ni wale wajumbe kwa zile nyakati saba za kanisa zinazofuatana. Hawatajwi kwa majina. Wao wameandikwa tu kama saba, mmoja kwa kila wakati. Tangu Wakati wa Efeso na kuendelea mpaka kwenye Wakati huu wa Laodikia kila mjumbe alileta ujumbe wa kweli kwa watu, bila kukosea kuliweka hilo Neno la Mungu katika wakati huo huo tu wa kanisa. Kila mmoja alishikilia hilo. Wao walikuwa thabiti katika uaminifu wao kwa ile nuru ya kwanza. Kwa kuwa kila wakati wa kanisa ulikuwa unawacha Mungu, mjumbe wake mwaminifu aliurudisha wakati huo kwenye Neno. Nguvu yao ilikuwa inatoka kwa Bwana la sivyo hawangeweza kamwe kuyastahimili mawimbi. Walikuwa salama wakiwa katika ulinzi Wake, kwa kuwa hakuna kitu kingaliweza kuwapokonya kutoka katika mkono Wake, na wala hakuna kitu kingaliweza kuwatenganisha na upendo wa Mungu, iwe ni maradhi, hatari, uchi, njaa, upanga, uzima au mauti. Walikuwa wamejisalimisha kwa dhati na kulindwa na nguvu Zake zote. Wao hawakuyajali mateso yaliyowakabili. Uchungu ama dhihaka hazikuwa ni kitu cho chote bali sababu ya kumpa Mungu utukufu ya kwamba walihesabiwa kwamba wanastahili kuteswa kwa ajili Yake. Na katika shukrani kwa ajili ya wokovu Wake waliangaza kwa nuru ya uhai Wake na wakadhihirisha mng'ao wa upendo Wake, subira, upole, kiasi, unyenyekevu, uaminifu. Na Mungu aliwaunga mkono kwa maajabu, ishara, na miujiza.

Walishtakiwa kuwa washupavu wa dini, na watakatifu wanaojifingirisha. Walishutumiwa na madhehebu na kudhihakiwa, bali walidumu waaminifu kwa Neno.

Sasa si vigumu kusimama na kudumisha kanuni za imani. Ni rahisi, kwa maana ibilisi yuko moja kwa moja nyuma ya hayo yote. Lakini ni jambo lingine kuwa mwaminifu kwa Neno la Mungu na kurudi kwenye yale ambayo Neno lilizaa hapo awali baada ya Pentekoste ni jambo lingine.

Si muda mrefu uliopita mtu fulani aliniambia ya kwamba kanisa Katoliki la Kirumi halina budi kuwa ndilo kanisa la kweli kwa kuwa limeshikilia kwa uaminifu yale linayoamini kwa miaka hii yote, na likaendelea kukua bila kubadilika. Sivyo ilivyo hata kidogo. Kanisa lo lote linaloungwa mkono na serikali, na kanuni zake za imani ambazo si Neno kamwe, na bila ya ya kuwa na huduma iliyodhihirishwa ya kumwasha ibilisi, hakika lingeweza kuendelea. Hicho hakikuwa kigezo. Lakini unapowazia juu ya kundi lile dogo ambalo washiriki wake walikatwa kwa misumeno, wakalishwa simba, wakateswa na kufukuzwa toka mahali hadi mahali na hata hivyo wakadumu waaminifu kwa Neno_sasa bila shaka huyo hana budi kuwa ni Mungu. Jinsi vile walivyopona katika vita vyao vya imani na wakazidi kusonga mbele: HUO ndio muujiza.

Na faraja hii si kwa ajili ya wale wajumbe saba wa wakati wa kanisa. Kila mwamini wa kweli yumo katika mkono wa Mungu na anaweza kunywa katika upendo Wake na nguvu Zake, na kupata fadhili zote za yale yote Mungu aliyo kwa mwamini. Yale Mungu anayompa mjumbe huyo, na jinsi anavyombariki na kumtumia hayo mjumbe, ni mfano kwa waamini wote juu ya wema Wake na malezi Yake kwa washiriki WOTE wa mwili Wake. Amina.

**6 Upanga wenye makali kuwili.**

*"Na katika kinywa Chake mlitoka upanga wenye makali kuwili."*

Katika Waebrania 4:12,

> *"Maana Neno la Mungu li hai, tena lina nguvu tena lina ukali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili, tena lachoma hata kuzigawanya nafsi na roho, na viungo na mafuta yaliyomo ndani yake tena li jepesi kuyatambua mawazo na makusudi ya moyo."*

Katika kinywa Chake kulitoka upanga mkali wenye makali kuwili ambao ni NENO LA MUNGU. Ufunuo 19:11-16,

> *"Kisha nikaona mbingu zimefunuka, na tazama, farasi mweupe; na Yeye aliyempanda linaitwa Mwaminifu na Wa-Kweli, Naye kwa haki ahukumu na kufanya vita.*
>
> *Na macho Yake yalikuwa kama mwali wa moto, na juu ya kichwa Chake vilemba vingi; naye ana jina lililoandikwa, asilolijua mtu, ila Yeye Mwenyewe.*
>
> *Naye amevikwa vazi lililochovywa katika damu: na Jina Lake aitwa Neno la Mungu.*
>
> *Na majeshi yaliyo mbinguni yakamfuata wamepanda farasi weupe, na kuvikwa kitani nzuri, nyeupe, na safi.*
>
> *Na upanga mkali hutoka kinywani Mwake, ili awapige mataifa kwa huo: Naye atawachunga kwa fimbo ya chuma: Naye anakanyaga shinikizo la mvinyo ya ghadhabu ya hasira ya Mungu Mwenyezi.*
>
> *Naye ana jina limeandikwa katika vazi Lake na paja Lake, MFALME WA WAFALME, NA BWANA WA MABWANA.*"

Yohana 1:48,

> *"Nathanaeli akamwambia, Umepataje kunitambua? Yesu akajibu akamwambia, Kabla Filipo hajakuita, ulipokuwapo chini ya mtini, nilikuona."*

Hilo hapo. Atakapokuja, Neno hilo litakuja dhidi ya mataifa yote na watu wote. Wala hakuna mtu atakayeweza kulipinga. Litafunua kilichokuwa katika kila moyo kama alivyofanya na Nathanaeli. Neno la Mungu litaonyesha ni nani aliyetenda mapenzi ya Mungu na ni nani hakuyatenda. Litafunua kazi za siri za kila mtu na ni kwa nini alizitenda. Litagawanya vipande-vipande. Hivyo ndivyo linavyosema katika Warumi 2:3,

> *"Wewe binadamu, uwahukumuye wale wafanyao hayo, na kutenda yayo hayo mwenyewe, je! wadhani ya kwamba utajiepusha na hukumu ya Mungu?"*

Ndipo inaendelea kusema jinsi Mungu atakavyowahukumu wanadamu. Hii hapa katika aya ya 5 hadi 17. Moyo mgumu usiotubu utahukumiwa. Kazi hizo zitahukumiwa. Makusudi yatahukumiwa. Hakutakuwako na upendeleo wo wote mbele za Mungu; lakini wote watahukumiwa kwa Neno hilo, hakuna atakayelieupuka. Wale ambao walisikia na hawangesikiliza watahukumiwa kwa yale waliyosikia. Wale

waliolitumainia wakisema wanaliamini, bali hawakulitimiza, watahukumiwa. Kila siri itatoka hadharani na kutangazwa kutoka juu ya nyumba. Loo, kweli tutaelewa historia wakati huo. Hakutakuwako na siri itakayosalia kutoka katika nyakati zote.

Lakini unajua ya kwamba Yeye anazifunua siri za mioyo ya wanaume na wanawake katika kizazi hiki tunachoishi? Ni nani mwingine angeweza kufunua siri za moyo ila Neno, Mwenyewe? Waebrania 4:12,

> *"Maana Neno la Mungu li hai, tena lina nguvu, tena lina ukali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili, tena lachoma hata kuzigawanya nafsi na roho, na viungo na mafuta yaliyomo ndani yake, tena li jepesi kuyatambua mawazo na makusudi ya moyo."*

Ni Neno. Linatenda yale liliyotumwa kutenda, kwa kuwa Hilo (Neno) limejaa nguvu. Ni Roho yule yule aliyekuwa katika Yesu (Neno) ambaye yuko tena katika kanisa katika wakati huu wa mwisho kama ishara ya mwisho akijaribu kuwaondoa watu watoke kwenye hukumu, kwa maana wale wanaomkataa Yeye (Neno) sasa tayari wamekuja hukumuni, wakimsulibisha upya. Waebrania 6:6,

> *"Wakaanguka baada ya hayo, haiwezekani kuwafanya upya tena hata wakatubu; kwa kuwa wamsulibisha Mwana wa Mungu mara ya pili kwa nafsi zao, na kumfedhehi kwa dhahiri."*

Sasa Paulo alisema ya kwamba Neno lilikuja katika nguvu na katika sauti. Neno lililohubiriwa kweli lilijidhihirisha. Kama upanga uwakao na kukata liliingia katika dhamira za watu, na kama kisu cha mpasuaji lilikata likaondoa magonjwa na kuwafungulia wafungwa. Kila mahali waamini hawa wa mwanzoni walipoenda, "Walienda wakihubiri Injili (Neno) na Mungu alithibitisha Neno hilo kwa ishara zilizofuata." Wagonjwa waliponywa, pepo walitolewa, nao walinena kwa lugha mpya. Hilo lilikuwa Neno likitenda kazi. Neno hilo halijashindwa kamwe katika vinywa vya Wakristo wanaoamini. Na katika wakati huu wa mwisho liko hapa likiwa na nguvu zaidi na likiwa kuu zaidi kuliko lilivyowahi kuwa katika bibi-arusi Neno wa kweli. Loo! enyi kundi dogo, enyi kusanyiko dogo, shikilieni Neno, jaza kinywa chako na moyo kwalo, na siku moja Mungu atakupa ule ufalme.

### 7 Uso Wake Kama Jua.

> *"Na uso Wake kama jua liking'aa kwa nguvu zake."*

Mathayo 17:1-13,

> *"Na baada ya siku sita Yesu akawatwaa Petro, na Yakobo, na Yohana nduguye, akawaleta juu ya mlima mrefu faraghani.*
>
> *Akageuka sura Yake mbele yao: uso Wake ukang'aa kama jua, mavazi Yake yakawa meupe kama nuru.*
>
> *Na, tazama, wakatokewa na Musa na Eliya wakizungumza Naye.*
>
> *Petro akajibu, akamwambia Yesu, Bwana, ni vizuri sisi kuwapo hapa: ukitaka, na tufanye hapa vibanda vitatu; kimoja Chako Wewe, na kimoja cha Musa na kimoja cha Eliya.*
>
> *Alipokuwa katika kusema, tazama, wingu jeupe likawatia uvuli: na tazama sauti ikatoka katika lile wingu, ikasema, Huyu ni Mwanangu mpendwa Wangu, ninayependezwa Naye; msikieni Yeye.*
>
> *Na wale wanafunzi waliposikia, walianguka kifulifuli, wakaogopa sana.*
>
> *Yesu akaja akawagusa, akasema, Inukeni, wala msiogope.*
>
> *Wakainua macho yao, wasione mtu, ila Yesu peke Yake.*
>
> *Na walipokuwa wakishuka mlimani, Yesu aliwaagiza, akasema, Msimwambie mtu ye yote habari ya ono hilo, hata Mwana wa Adamu atakapofufuka katika wafu.*
>
> *Wanafunzi Wake wakamwuliza, wakisema, Basi kwa nini waandishi hunena ya kwamba imempasa Eliya kuja kwanza?*
>
> *Naye Yesu akajibu akawaambia, Kweli Eliya yuaja kwanza, naye atatengeneza yote.*
>
> *Ila nawaambia, ya kwamba Eliya amekwisha kuja, wasimtambue, lakini wakamtenda yote waliyotaka. Vivyo hivyo, Mwana wa Adamu Naye yuaenda kuteswa kwao.*
>
> *Ndipo wale wanafunzi walipofahamu ya kuwa amesema nao habari za Yohana Mbatizaji."*

Sasa katika Mathayo 16:28, ikitangulia Mathayo 17:1-13, Yesu alikuwa amesema,

*"... Pana watu katika hawa, wasimamao hapa, ambao hawataonja mauti kabisa, hata watakapomwona Mwana wa Adamu akija katika ufalme Wake."*

Na wale mitume watatu kweli waliona jambo hilo_utaratibu wa kuja Kwake mara ya pili. Walimwona amegeuka sura kule juu ya mlima. Mavazi Yake yakawa meupe sana na uso Wake uling'aa kama jua katika nguvu Zake. Na pale alipotokea, walisimama Musa na Eliya upande huu na upande huu. Hivyo ndivyo hasa anavyokuja tena. Hakika Eliya atakuja kwanza na kuigeuza mioyo ya watoto (bibi-arusi) kurudi kwa baba zao wa Fundisho la Neno la baba zao Mitume. Malaki 4:5,6,

*"Angalieni, nitawapelekea Eliya nabii kabla haijaja siku ile ya Bwana iliyo kuu na kuogofya:*

*Naye ataigeuza mioyo ya baba iwaelekee watoto wao, na mioyo ya watoto iwaelekee baba zao, ili nisije nikaipiga dunia kwa laana."*

Israeli tayari ni taifa. Limeimarishwa sasa pamoja na majeshi yake, jeshi la majini, mfumo wa posta, bendera, na yote yanayohusu taifa. Lakini bado hakuna budi kutimizwa kwa Maandiko yanayosema, "...ama taifa laweza kuzaliwa mara moja..." Isaya 66:8. Siku hiyo inakuja hivi karibuni. Mtini umechanua machipukizi yake. Waisraeli wanamngojea Masihi. Wanamtarajia na matarajio yao yako karibu kutimizwa. Israeli watazaliwa upya Kiroho, kwa kuwa Nuru yake na Uzima wake viko karibu kufunuliwa kwake.

Katika Ufunuo 21:23,

*"Na mji ule hauhitaji jua, wala mwezi, kuuangaza: kwa maana utukufu wa Mungu huutia nuru, na taa yake ni Mwana-Kondoo."*

Huu ni Yerusalemu Mpya. Mwana-Kondoo atakuwa katika mji huo, na kwa sababu ya uwepo Wake, hakutahitajika nuru: Jua halitachomoza na kuwaka kwake, kwa kuwa Yeye ndiye Jua na Nuru yake, Yeye Mwenyewe. Mataifa watakaoingia ndani yake watatembea katika nuru Yake. Je! wewe hufurahi ya kwamba siku hiyo imetufikia? Yohana aliona siku hiyo ikija. Hata hivyo, Bwana Yesu, njoo upesi!

Malaki 4:1-3,

*"Kwa maana, angalieni, siku ile inakuja, inawaka kama tanuru: na watu wote wenye kiburi, naam, nao wote watendao uovu, watakuwa makapi: na siku ile inayokuja itawateketeza, asema Bwana wa Majeshi, hata haitawaachia shina wala tawi.*

*Lakini kwenu ninyi mnaolicha Jina Langu Jua la Haki litawazukia, lenye kuponya katika mbawa Zake; nanyi mtatoka nje, na kucheza-cheza kama ndama wa mazizini.*

*Nanyi mtawakanyaga waovu; maana watakuwa majivu chini ya nyayo za miguu yenu katika siku ile niifanyayo, asema Bwana wa Majeshi."*

Hilo hapo tena. JUA likiangaza katika nguvu zake zote. Loo, nguvu za Mwana wa Mungu zikiangaza katikati ya vile vinara vya taa saba vya dhahabu. Huyo hapo amesimama, Hakimu, Yeye aliyeteseka na kufa kwa ajili yetu. Alichukua hasira ya hukumu ya Kiungu juu Yake Mwenyewe. Yeye anakanyaga shinikizo la mvinyo ya ghadhabu ya hasira ya Mungu peke Yake. Kama tulivyokwisha kusema, kwa mwenye dhambi sauti Yake ni kama sauti ya maporomoko ya maji ama mawimbi meupe yakitwanga katika mawimbi ya mauti kwenye ufuko wenye miamba. Lakini kwa mtakatifu, sauti Yake ni kama sauti ya kijito kinachoimba kwa utamu unapolala starehe, umeridhika katika Kristo. Akiangaza juu yetu kwa miali Yake ya upendo ya joto, Yeye anasema, "Usiogope, Mimi ndimi Niliyekuwako, Niliyeko, Ninayekuja; Mimi ni Mwenyezi. Hakuna mwingine ila Mimi. Mimi ni Alfa na Omega, ni YOTE." Yeye ndiye Ua la Uwandani, Nyota Yenye Kung'aa ya Asubuhi. Yeye ndiye mzuri sana kuliko elfu kumi nafsini mwangu. Naam, siku hiyo kuu iko karibu kupambazuka na Jua la Haki litazuka lenye kuponya katika mbawa Zake.

**KRISTO ALIYE MSHINDI**

Ufunuo 1:17,18,

*"Nami nilipomwona, nalianguka miguuni Pake kama mtu aliyekufa. Akaweka mkono Wake wa kuume juu yangu, akisema, Usiogope, Mimi ni wa Kwanza na wa Mwisho,*

*Na aliye hai; nami nilikuwa nimekufa, na tazama, ni hai hata milele na milele, Amina; Nami ninazo funguo za mauti, na za kuzimu."*

Hakuna mwanadamu aliyeweza kustahimili matokeo kamili ya ono hilo. Nguvu Zake zikiwa zimekwisha kabisa, Yohana alianguka miguuni Pake kama aliyekufa. Lakini mkono wa Bwana katika upendo ukamgusa, na sauti ya baraka ikasema, "Usiwe na hofu. Usiogope. Mimi ni wa Kwanza na wa Mwisho. Mimi Ndimi Aliye hai, Nami nalikuwa nimekufa; na, tazama ni hai hata milele hata na milele." Kuna nini cha kuogopa? Ile hukumu iliyomshukia pale msalabani, kaburini, na wakati aliposhuka, ilikuwa ni kwa ajili yetu. Yeye alichukua uchungu wote wa jeraha la dhambi na kwa hiyo sasa hakuna hukumu ya adhabu kwa hao walio

katika Kristo Yesu. Mnaona kwa hakika "Wakili" wetu ndiye "Hakimu". Yeye ni "Wakili" na "Hakimu." Kama Hakimu "kesi imetatuliwa"_imekwisha. Kwa hiyo sasa basi hakuna hukumu ya dhambi. Kwa nini kanisa liogope? Ni ahadi gani Yeye amepata kushindwa kuidhihirisha mbele zetu? Kwa nini liogope adhabu au mauti? Yote yameshindwa. Huyu hapa yule mshindi mkuu. Yupo hapa Mmoja Ambaye ameshinda ulimwengu wa mambo yanayoonekana na yasiyoonekana. Si kama Alekizada, aliyeushinda ulimwengu akiwa na umri wa miaka thelathini na mitatu na hakujua njia nyingine yo yote ya kwenda akashinde zaidi, kwa hiyo akafa akiwa mateka wa dhambi na maisha ya uasherati. Si kama Napolioni, aliyeshinda Ulaya nzima lakini mwishowe akashindwa hapo Waterloo na kuhamishwa akapelekwa Elba, akajikuta tu ameshindwa. Lakini hakuna kitu kingeweza kumshinda Kristo. Yeye aliyeshuka sasa amepaa juu ya yote, na amepewa Jina lipitalo kila jina. Naam, Yeye alishinda kifo, kuzimu, na kaburi, naye ana funguo zake. Kile anachofungulia kimefunguliwa, na kile anachofunga kimefungwa. Hakuna kubadilishwa kwa jambo hilo. Hakukuwa na mshindi kabla Yake wala hakuna mwingine zaidi ya Yeye. Yeye pekee ndiye Mwokozi, Mkombozi. Yeye ndiye Mungu Pekee: na "Bwana Yesu Kristo" ndilo Jina Lake.

"Usiogope, Yohana. Msiogope, enyi kundi dogo. Yote niliyo, wewe ni mrithi wake. Nguvu zangu zote ni zako. Uwezo Wangu ni wenu ninaposimama katikati yenu. Sikuja kuleta hofu na kushindwa, bali upendo na ujasiri na uwezo. Nimepewa mamlaka yote nanyi mnaweza kuyatumia. Wewe nena Neno nami nitalitimiza. Hilo ndilo agano Langu na haliwezi kushindwa kamwe."

**ZILE NYOTA SABA NA VINARA VYA TAA**

Ufunuo 1:20,

> *"Siri ya zile nyota saba ulizoziona katika mkono Wangu wa kuume, na ya vile vinara saba vya dhahabu. Zile nyota sba ni malaika (wajumbe) wa yale makanisa saba: na vile vinara saba unavyoviona ni makanisa saba."*

Tayari tumegundua ukweli wa siri hizi mbili. Loo, hatujafunua hawa wajumbe saba walikuwa ni nani, bali kwa msaada wa Mungu tutafanya hivyo na siri hiyo itatimizwa. Zile nyakati saba tunazijua. Zimeorodheshwa katika Neno, na tutashughulikia kila mmoja kusudi tufikie wakati huu wa mwisho tunaoishi.

Lakini katika kutupia jicho la kufunga sura hii, tunamwona Yeye anaposimama pale katikati ya vinara vya taa saba vya dhahabu ameshika nyota saba katika mkono Wake wa kuume. Loo! ni jambo la kusisimua moyo sana kumwona Yeye amesimama pale katika Uungu Wake Mkuu. Yeye ndiye Hakimu, Kuhani, Mfalme, Tai, Mwana-Kondoo, Simba, Alfa, Omega, Mwanzo na Mwisho, Baba, Mwana, Roho Mtakatifu, Yeye Aliyekuwako, Aliyeko, Anayekuja, Mwenyezi, YOTE KATIKA YOTE. Huyo hapo, Mwanzilishi na Mkamilishaji. Mwana-Kondoo Aliyestahiliye! Yeye alithibitish ustahilifu Wake kati Yeye Mwenyewe alipoununua wokovu wetu. Sasa Yeye anasimama katika nguvu Zake zote na utukufu Wake wote na vitu vyote vimewekwa Kwake kama Hakimu.

Naam, Huyo hapo amesimama katikati ya vinara vya taa, akiwa na zile nyota mkononi Mwake. Ni usiku, kwa sababu huo ndio wakati tunapotumia taa kwa ajili ya nuru, na hapo ndipo nyota zinapoonekana zikiwaka na kurudisha nuru ya jua. Na ni giza. Kanisa linatembea kwa imani gizani. Bwana wake aliondoka hapa duniani lakini Roho Mtakatifu angali anaangaza kupitia katika kanisa, akitoa nuru kwa ulimwengu huu wa kale uliolaaniwa na dhambi. Na nyota hizo zinaakisi nuru Yake pia. Nuru pekee zilizo nayo ni nuru Yake. Ni giza jinsi gani—ni baridi kiroho jinsi gani. Hata hivyo wakati anapoingia katikati kuna nuru na joto, na kanisa limepewa nguvu na kupitia Kwake linatenda kazi alizozifanya.

Loo, ili kwamba tupate kumwona kidogo Yeye kama vile Yohana alivyofanya. Tunapaswa kuwa ni watu wa aina gani, tukiwa tumesimama mbele Zake siku hiyo!

Kama hujampa Yeye maisha yako tayari, hebu uelekeze moyo wako kwa Mungu wakati huu, na upige magoti papo hapo ulipo, na uombe msamaha Wake kwa ajili ya dhambi zako, na uyasalimishe maisha yako Kwake. Ndipo tutajaribu kuzikaribia zile Nyakati Saba za Kanisa pamoja; na tunapofanya hivyo ninaomba ya kwamba Mungu atamsaidia mtumishi huyu asiyestahili kulifunua Neno Lake kwako.

www.messagehub.info

Mahubiri Na

William Marrion Branham

"... katika siku za sauti ..." Ufu. 10:7